ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*Supplement No. 25* *1st July, 2022*

***SPECIAL SUPPLEMENT***

*to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.25. Vol.103 dated 1st July, 2022*
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 478P la tarehe 01/07/2022

SHERIA YA MICHEZO YA KUBAHATISHA,
(SURA YA 41)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 85)*

KANUNI YA MICHEZO YA KUBAHATISHA MTANDAONI, 2022

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina na matumizi.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MASHARTI YA LESENI

*GN NO. 478P (Tangazo Linaendelea)*

3. Vigezo vya kupatiwa leseni ya michezo ya kubahatisha.

SEHEMU YA TATU
UTOAJI WA LESENI

4. Maombi ya leseni ya michezo ya kubahatisha mtandaoni.
5. Uchunguzi na gharama za uchunguzi.
6. Masharti yanayoambatana na leseni.
7. Maombi ya leseni ya mtoa huduma.
8. Maombi ya leseni ya mfanyakazi maalum.

SEHEMU YA NNE
UENDESHAJI

9. Kuhifadhi seva.
10. Wajibu wa mtoa huduma.
11. Mipango ya dharura.
12. Kituo cha usimamizi.
13. Utambuzi wa mchezaji.
14. Usajili wa mchezaji.
15. Kukataa kusajili.
16. Akaunti ya kushiriki.
17. Mmiliki wa leseni kutumia akaunti ya mchezaji.
18. Udhibiti wa akaunti ya mchezaji.
19. Michezo iliyokatizwa au kutokufanyika.

SEHEMU YA TANO
TUZO

20. Tuzo ya fedha na isiyo ya fedha.
21. Tuzo isiyo ya fedha ambayo haijadaiwa.
22. Madai ya tuzo ambayo haijalipwa.
23. Kutaifishwa kwatuzo ambazo hazijachukuliwa.
24. Kuzuia tuzo.
25. Tuzo kuwekwa wazi.

SEHEMU YA SITA
MIFUMO YA UDHIBITI

26. Uanzishaji wa mifumo ya udhibiti.
27. Viwango, vipimo na miongozo.
28. Uidhinishaji wa mifumo ya udhibiti.
29. Kushindwa kuripoti mabadiliko.
30. Uamuzi.
31. Maelekezo ya kubadili mfumo wa udhibiti.
32. Viwango vya usanifu, matumizi na utunzaji wa tovuti.
33. Viwango vya ulinzi, ufikiaji na utunzaji.

SEHEMU YA SABA
UDHIBITI WA NDANI

34. Uanzishaji wa utaratibu wa udhibiti wa ndani.
35. Uidhinishaji wa utaratibu wa udhibiti wa ndani.
36. Urekebishaji wa utaratibu wa ndani ulioidhinishwa.

SEHEMU YA NANE
UTOAJI TAARIFA KWA MIAMALA SHUKU

37. Kanuni na taratibu za miamala shuku.
38. Wajibu wa kuripoti miamala shuku.

SEHEMU YA TISA
ULINZI WA MCHEZAJI

39. Ulinzi kwa watoto.
40. Urudishaji wa fedha.
41. Usajili.
42. Vigezo na masharti.
43. Ukiukwaji wa kanuni.
44. Utenganishaji wa akaunti.
45. Marekebisho ya akaunti ya mchezaji.
46. Utoaji wa mikopo.

*GN NO. 478P (Tangazo Linaendelea)*

SEHEMU YA KUMI
WAJIBU WA KUCHEZA KISTAARABU

47. Notisi ya onyo.
48. Kujiondoa.
49. Taarifa za mchezaji kuondolewa.
50. Ukomo wa kubeti au dau.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
KUMBUKUMBU ZA HESABU NA RITANI

51. Kumbukumbu za hesabu.
52. Taarifa za fedha zilizokaguliwa.
53. Taratibu za ukaguzi wa Bodi.
54. Ritani na uwasilishaji wa ritani ya kila mwezi.
55. Taarifa za fedha za uongo au za kupotosha.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
MASHARTI YA JUMLA

56. Matangazo kwenye shughuli zenye leseni.
57. Kanuni kutangazwa kwa Kiswahili na Kiingereza.
58. Dhamana ya benki.
59. Dhamana.
60. Utoaji wa taarifa bila ruhusa.
61. Ushughulikiaji wa malalamiko.
62. Usuluhisiwa migogoro.
63. Utoaji wa taarifa kwa vitendo visivyo halali.
64. Adhabu.

---

**JEDWALI**

---

*GN NO. 478P (Tangazo Linaendelea)*
TANGAZO LA SERIKALI NA. 478P la tarehe 01/07/2022

SHERIA YA MICHEZO YA KUBAHATISHA,
(SURA YA 41)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 85)*

KANUNI ZA MICHEZO YA KUBAHATISHA MTANDAONI, 2022

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina na matumizi

**1**.-(1) Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Michezo ya Kubahatisha Mtandaoni, 2022.

(2) Kanuni hizi zitatumika kwa michezo yote ya kimtandao iliyopewa leseni chini ya Sheria.

Tafsiri

**2**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa muktadha unahitaji vinginevyo-

Sura ya 41

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Michezo ya Kubahatisha;

"muombaji" maana yake ni mtu yeyote anayeomba au anayetaka kuomba leseni ya michezo ya kubahatisha, leseni ya mtengenezaji au mwendeshaji au msambazaji, usajili au kutafuta kukubalika chini ya masharti ya Sheria, au idhini ya kitendo chochote au muamala ambao leseni ya Bodi ya maduka ya michezo ya kubahatisha, leseni ya bahati nasibu, inatakiwa au kutolewa chini ya masharti ya Sheria;

"wakala aliyeidhinishwa" maana yake ni mtu au watu walioidhinishwa na Bodi kutekeleza kazi yoyote

iliyoainishwa katika Sheria au Kanuni hizi, kwa ajili na kwa niaba ya Bodi na inajumuisha mamlaka iliyoteuliwa;

"benki" maana yake ni taasisi inayojishughulisha na biashara ya benki;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ya Tanzania iliyoanzishwa na kifungu cha 4(1) cha Sheria;

"mifumo ya udhibiti" maana yake ni programu, mianzi laini, mianzi ngumu, mifumo na viwango vinavyoathiri matokeo ya shughuli ya michezo ya kubahatisha iliyoidhinishwa;

"michezo ya kubahatisha mtandaoni" maana yake ni shughuli ya michezo ya kubahatisha inayofanywa kwa kutumia kifaa kilichounganishwa kwa njia ya mtandao, au aina nyingine yoyote ya kielektroniki au teknolojia nyingine inayowezesha mawasiliano;

"akaunti iliyoteuliwa" maana yake ni akaunti iliyoteuliwa na mchezaji, inayoshikiliwa na benki au taasisi ya fedha kwa ajili ya kuhamisha fedha kuhusiana na michezo ya kubahatisha ya mtandao, na ambayo haitahusisha uhamisho wa fedha taslimu;

"akaunti ya mchezaji" maana yake ni akaunti inayomilikiwa na mchezaji, ambayo mmiliki wa leseni ana haki ya kutoa dau;

"tatizo litokanalo na kucheza michezo ya kubahatisha" maana yake ni ushiriki wa mara kwa mara katika shughuli ya michezo ya kubahatisha ambayo inaweza kusababisha madhara ya kisaikolojia, kiutendaji na kiuchumi, kwake au familia.

## SEHEMU YA PILI
## MASHARTI YA LESENI

Vigezo vya

**3.** Katika kuzingatia kama mtu anafaa kwa

kupatiwa leseni ya michezo ya kubahatisha

madhumuni ya kupewa leseni yoyote kwa mujibu wa Sheria au Kanuni hizi, hakuna mtu atakayepewa leseni ya michezo ya kubahatisha isipokuwa mtu huyo-

(a) hajawahi kunyimwa leseni ya michezo ya kubahatisha na mamlaka hii au nyinginezo;

(b) hajawahi kusitishiwa au kufutiwa leseni ya michezo ya kubahatisha na mamlaka hii au nyinginezo;

(c) hajawahi kuondoa maombi ya leseni yoyote ya michezo ya kubahatisha popote kwa sababu zozote;

(d) ana majengo ya michezo ya kubahatisha ambayo yanaonekana yanafaa na Bodi;

(e) anazingatia masharti yote ya Sheria na Kanuni hizi;

(f) hajatiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai linalohusisha ulaghai au kukosa uaminifu;

(g) ana uthibitisho wa uwezo wa kifedha za kutosha unaomuwezesha kutekeleza majukumu yote na kutoa mtaji wa kutosha wa kugharamia uendeshaji wa shughuli za michezo ya kubahatisha; na

(h) ana teknolojia na vifaa vinavyohitajika ambavyo vimejaribiwa na kuthibitishwa na taasisi iliyoidhinishwa.

## SEHEMU YA TATU
## UTOAJI WA LESENI

Maombi ya leseni ya michezo ya kubahatisha mtandaoni

**4.**-(1) Maombi chini ya kanuni hii yatawasilishwa kwa Bodi katika nakala mbili za fomu kwa namna iliyoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi au kwa njia ya kielektroniki.

(2) Maombi yatakayofanywa chini ya kanuni ndogo ya (1) yatakuwa na taarifa zote zilizoombwa kwenye fomu na kuambatishwa na-

(a) mpango wa biashara;

*GN NO. 478P (Tangazo Linaendelea)*

(b) nakala ya katiba na kanuni za kampuni;

(c) nakala ya hati ya usajili wa kampuni iliyothibitishwa;

(d) uthibitisho wa mtaji wa kutosha wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi;

(e) uthibitisho wa uraia wa kila mwanahisa, mkurugenzi na mfanyakazi maalumu, ikijumuisha wasifu wa kina kwa kila mwanahisa, mkurugenzi na mfanyakazi maalumu, nakala ya ukurasa wa hati ya kusafiria yenye maelezo ya mmiliki na picha ya pasipoti;

(f) fomu ya tamko iliyoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi kwa kila mkurugenzi au mwanahisa mwenye asilimia tano au zaidi ya umiliki au udhibiti wa maslahi katika taasisi inayoomba;

(g) endapo mwombaji ni kampuni, itawasilisha taarifa ya fedha iliyokaguliwa hivi karibuni;

(h) hati ya uthibitisho wa kulipa kodi kutoka kwa mamlaka ya mapato ya nchi anakotoka mwombaji mgeni na hati ya uthibitisho wa kulipa kodi inayotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwombaji wa ndani, na kwa kila mwanahisa, mkurugenzi na mfanyakazi maalumu, pale inapohusika;

(i) maelezo kutoka kwa watu wawili, ambao sio ndugu, wakithibitisha tabia njema ya kimaadili na wajibu wa kifedha wa mwanahisa na wakurugenzi na maafisa waandamizi wanaopendekezwa wakati wa maombi;

(j) azimio la Bodi ya Wakurugenzi ya mwombaji kuwekeza Tanzania;

(k) fomu ya ahadi ya kupinga rushwa;

(l) miongozo ya kucheza kwa ustaarabu;

(m) fomu za maombi zilizoainishwa katika

*GN NO. 478P (Tangazo Linaendelea)*

Kanuni hizi, kwa kila mkurugenzi wa mwombaji au mwanahisa mwenye asilimia tano au zaidi ya umiliki au udhibiti wa maslahi katika taasisi inayoomba;

TS. Na. 385 la 2003

(n) ada ya maombi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kanuni za Michezo ya Kubahatisha;

(o) taarifa za kina kuhusu mtoa huduma, muundo, vifaa na huduma zitakazotolewa kwa mmiliki wa leseni; na

(p) ufafanuzi wa teknolojia na chanzo chake.

Uchunguzi na gharama za uchunguzi

**5.-**(1) Baada ya kupokea maombi, chini ya kanuni ya 4(1), Bodi itafanya uchunguzi au kuhitaji kuwasilishwa kwa tamko au taarifa zaidi kama itakavyoona inafaa ili kuwezesha upekuzi yakinifu wa maombi hayo.

(2) Mtu yeyote ambaye atawasilisha nyaraka kwa Bodi kuhusiana na uchunguzi au upekuzi wowote ataweka kumbukumbu kamili na ya kina ya nyaraka zote.

(3) Baada ya kuwasilishwa, nyaraka zitakuwa sehemu ya mali ya Bodi na zitachukuliwa kuwa ni siri.

(4) Waombaji wote wa leseni, isipokuwa leseni ya mfanyakazi msaidizi, atalipa gharama za uchunguzi kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(5) Pamoja na gharama za uchunguzi, waombaji wote watalipa kwa Bodi gharama halisi zifuatazo zilizotumika katika kufanya uchunguzi wa awali-

(i) usafiri na gharama zinazohusiana;

(ii) gharama muhimu za uendeshaji wa ofisi mpaka ukamilishwaji wa zoezi la upekuzi na uchunguzi.

(6) Kabla ya uchunguzi wowote kufanyika, kila mwombaji atalipa kwa Bodi kiasi cha fedha ambacho kinaweza kutosha kwa ajili ya zoezi hilo.

(7) Pale ambapo kiasi kilichowekwa kwa ajili ya

kugharamia uchunguzi kinakaribia sifuri au kinatazamiwa kufikia sifuri kutokana na sababu zinazotarajiwa au zinazofahamika ambazo zitatokea hapo baadaye, Bodi itawasilisha maombi ya kuongeza fedha zaidi kwa ajili ukamilishwaji wa zoezi la uchunguzi.

(8) Zoezi la uchunguzi linaweza kusitishwa hadi fedha zaidi zitakapopokelewa.

(9) Pale ambapo mwombaji anapinga gharama yoyote ya uchunguzi, au uhitaji wa kuongeza fedha zaidi, mwombaji anaweza kuomba ahueni kutoka kwa Bodi, kwa amri ya tamko au hoja nyingine inayofaa, kuhusu masuala yanayobishaniwa.

(10) Ndani ya siku tisini baada ya kukamilika kwa uchunguzi, bakaa ya gharama za uchunguzi itarejeshwa kwa mwombaji ikiambatana na taarifa ya gharama zilizotolewa.

(11) Leseni haitatolewa hadi malipo ya kiasi kamili cha salio linalopungua kimepokelewa kutoka kwa mwombaji.

TS. Na. 385 la 2003

(12) Baada ya uchunguzi mmiliki wa leseni, atapewa hati ya kufaa iliyoainishwa katika Jedwali la Kanuni za Michezo ya Kubahatisha, baada ya malipo ya shilingi milioni moja.

Masharti yanayoambatana na leseni

**6.** Bodi inaweza kuweka masharti kwa leseni iliyotolewa chini ya Sheria kuhusiana na:

(a) viwango vya kiufundi na namna ya uendeshaji;
(b) vipimo vya kiufundi na viwango vya mianzi laini na vifaa;
(c) asili na vipimo vya mfumo wa udhibiti na taratibu za ndani;
(d) kuendesha akaunti ya benki nchini;
(e) kutumia kifaa cha michezo ya kubahatisha au teknolojia iliyoithibitishwa na wakala aliyeidhinishwa;

*GN NO. 478P (Tangazo Linaendelea)*

(f) wajibu wa kutuma miamala ya michezo ya kubahatisha kwenye mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji na udhibiti wa michezo ya kubahatisha;

(g) wajibu wa kuwazuia watu walio chini ya umri wa miaka kumi na nane kushiriki katika shughuli za michezo ya kubahatisha;

(h) wajibu wa kuweka dhamana kwa Bodi;

(i) wajibu wa kuhamasisha uchezaji wa kistaarabu wa michezo ya kubahatisha;

(j) udhibiti wa matangazo; na

(k) wajibu wa kuzingatia matakwa ya sheria na maelekezo yanayotolewa na Bodi mara kwa mara.

Maombi ya leseni ya mtoa huduma

**7**. Mwombaji wa leseni ya mtoa huduma atawasilisha taarifa zifuatazo-

(a) hati ya usajili;

(b) wasifu wa kampuni;

(c) hati za uthibitishaji wa bidhaa au huduma; na

(d) nakala ya leseni iliyothibitishwa na kutolewa katika mamlaka ya kigeni ambapo mwombaji anatoa huduma kama hiyo.

Maombi ya leseni ya mfanyakazi maalumu
TS. Na. 385 la 2003

**8**.-(1) Maombi ya leseni ya mfanyakazi maalumu yatawasilishwa kwa Bodi katika fomu kwenye nakala mbili kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Michezo ya Kubahatisha.

(2) Maombi yaliyofanywa chini ya kanuni hii yataambatishwa na-

(a) barua kutoka kwa mwombaji au mmiliki wa leseni kwenda kwa Bodi ikiwa na yafuatayo:

(i) nafasi inayopendekezwa;

(ii) majukumu na wajibu yanayoambatana na nafasi inayopendekezwa;

(iii) sifa alizonazo; na

(iv) aina ya mafunzo aliyopokea.

TS. Na. 385 la 2003

(b) ada ya maombi ya leseni ya mfanyakazi maalumu kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Michezo ya Kubahatisha;

(c) fomu ya tamko iliyojazwa kikamilifu kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Michezo ya Kubahatisha;

(d) wasifu wa mleta maombi wenye wadhamini wawili;

(e) barua kutoka kwa mwajiri wa awali;

(f) nakala ya Kitambulisho cha Taifa kwa mwombaji wa ndani au hati ya kusafiria kwa mwombaji mgeni;

(g) picha mbili za pasipoti za hivi karibuni; na

(h) taarifa nyingine yoyote kama itakavyohitajika na Bodi.

## SEHEMU YA NNE
## UENDESHAJI

Kuhifadhi seva

**9**.-(1) Mmiliki wa leseni atakuwa na seva ya msingi ndani ya Tanzania Bara.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1) na baada ya idhini ya Bodi, seva ya msingi inaweza kuhifadhiwa nje ya Tanzania Bara kwa muda utakaoainishwa na Bodi:

Isipokuwa kwamba, kwa kipindi ambacho seva ya mmiliki wa leseni imehifadhiwa nje ya Tanzania Bara, mmiliki wa leseni atahifadhi seva inayofanana na ile iliyopo Tanzania Bara.

(3) Baada ya kumalizika kwa muda ulioainishwa na Bodi chini ya kanuni ndogo ya (2), seva ya msingi ya mmiliki wa leseni itawekwa Tanzania Bara.

(4) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (2), pale ambapo seva ya msingi imehifadhiwa nje ya Tanzania Bara, mfumo wa udhibiti wa fedha utakuwa ndani ya Tanzania Bara.

(5) Mmiliki wa leseni atahakikisha kuwa

masuala yanayohusiana na eneo, jengo, ulinzi na usalama wa jengo, uokoaji wa maafa na taratibu za ndani za mazingira ya kuhifadhia yameshughulikiwa ipasavyo.

(6) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (5), mmiliki wa leseni atazingatia kila mojawapo ya vipengele vifuatavyo-

(a) kwenye eneo-

(i) ukaribu wa usambazaji wa teknolojia za habari, mawasiliano ya simu na bidhaa au huduma zinazohusiana;

(ii) ukaribu wa huduma kwa mahitaji ya mtumiaji, biashara au mfanyakazi;

(iii) uhakika wa upatikanaji wa nishati ya umeme na huduma za mawasiliano ya simu;

(iv) upatikanaji wa kipimo data;

(v) urahisi wa kufikia jengo ikiwa ni pamoja na eneo la maegesho na uzingatiaji wa msongamano; na

(vi) wakaazi walio karibu na majengo au ofisi;

(b) kwenye miundombinu ya jengo-

(i) chumba cha seva kukidhi viwango vya kimataifa;

(ii) upungufu wa nishati ya umeme na milisho ya mawasiliano ya simu;

(iii) vifaa vya nishati vya nje ya mkondo wa umeme ambavyo ni pamoja na ugavi wa nishati usiokatizwa na jenereta;

(iv) idadi ambayo jenereta litahitaji kujazwa mafuta tena na mipango iliyopo;

(v) uwashaji wa vifaa vya nishati vya nje ya mkondo wa umeme;

(vi) ni mara ngapi vifaa vya nishati vya

nje ya mkondo wa umeme hujaribiwa;

(vii) mfumo wa dharura wa taa;

(viii) ufikiwaji wa lifti na sehemu za kupakilia;

(ix) utoshelezi wa mifumo ya ndani ya nyaya, nyaya au matoleo;

(x) karakana inayojitosheleza na nafasi ya ofisi kwa ajili ya wateja;

(xi) eneo lililotengwa kwa ajili ya kutolea ufafanuzi kwa wateja; na

(xii) upatikanaji wa satelaiti;

(c) ulinzi na usalama wa jengo-

(i) mipaka ya uzio;

(ii) umuhimu wa kutumia walinzi;

(iii) udhibiti wa kuingia kielektroniki au fizikali au vinginevyo;

(iv) mifumo ya kengele;

(v) matokeo ya majaribio ya mifumo ya usalama inapotokea hitilafu ya umeme;

(vi) kamera za kufuatilia eneo zima, eneo linalolindwa na maeneo ya karibu;

(vii) ufuatiliaji wa watumishi katika maeneo muhimu;

(viii) hatua za kuzuia ufuatiliaji kwenye tovuti au vifaa vya kusikiliza vya mbali, ufuatiliaji wa kielektroniki wa shughuli za kompyuta;

(ix) wakandarasi wanaotumika hasa wanaofanya usafi;

(x) ufikiaji wa vifaa vya usambazaji na upatikanaji wa mawasiliano;

(xi) ufikiaji wa mtambo na vyumba vya vifaa ikiwemo vingine vya lifti na kiyoyozi;

(xii) ujenzi wa ukuta wa nje na wa ndani;

*GN NO. 478P (Tangazo Linaendelea)*

(xiii) ubora wa vitasa;

(xiv) kiwango cha usalama cha milango, madirisha, sehemu za dharura za moto, sehemu ya kupokelea mizigo na sehemu nyingine za kuingilia;

(xv) mfumo wa kuzima moto;

(xvi) kiyoyozi;

(xvii) ulinzi wa taa;

(xviii) mahitaji ya usalama na afya mahali pa kazi;

(d) uokoaji wa maafa-

(i) uwezo wake;

(ii) mpango wa mwendelezo wa biashara;

(e) katika taratibu za ndani-

(i) kanuni na udhibiti wa kuingia kwa wafanyakazi na wageni;

(ii) utunzaji wa rejista au kitabu cha kumbukumbu za kuingia;

(iii) kushughulikia arifa za kengele za kiufundi na usalama;

(iv) idhini ya wakandarasi;

(v) maombi ya dharura ya kuingia;

(vi) ukaguzi wa kawaida wa usalama au upekuzi;

(vii) utendaji kazi wa wakati wote au utaratibu nje ya saa;

(viii) uwepo wa mfanyakazi maalumu au upatikanaji wake anapohitajika;

(ix) taratibu za dharura zinazojumuisha uokoaji na moto; na

(x) taarifa za mtu binafsi, kibali na mafunzo.

(7) Seva ya msingi na mifumo ya udhibiti wa fedha itakuwa angalau na taarifa zote zinazohusiana na wachezaji wote ikiwa ni pamoja na historia ya mchezo, historia ya fedha na madeni ya sasa.

(8) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (4) "mfumo wa udhibiti wa fedha" maana yake ni mfumo wa kompyuta wenye mfanano wa wakati halisi wa fedha na taarifa ya mchezaji kutoka katika shughuli ya mchezo wa kubahatisha mtandaoni.

Wajibu wa mtoa huduma

**10**.-(1) Mtoa huduma atawasilisha mpango wa mazingira ya utunzaji pamoja na ukandarasi wa topolojia kwa ajili ya kuidhinishwa na Bodi kabla ya uendeshaji.

(2) Bodi itamtaka mtoa huduma ya uhifadhi kufanya maombi ya cheti cha kufaa.

Mipango ya dharura

**11**.-(1) Mmiliki wa leseni ataweka mipango ya dharura na muendelezo wa biashara ili kuhakikisha uwezo wa kuendesha biashara kwa msingi unaoendelea na kupunguza hasara mbaya kutokana na muingiliano wa kibiashara.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mipango hiyo itakuwepo kwa ajili ya michakato yote muhimu ya biashara na itazingatia aina tofauti za matukio yanayokubalika.

(3) Bila kujali kanuni ndogo ya (2) umakini utaelekezwa katika uwezo wa kurejesha kumbukumbu za kielektroniki au za nakala ngumu ambazo ni muhimu kwa kurudisha biashara upya.

(4) Mmiliki wa leseni mara kwa mara atapitia mipango yake ya kujikwamua katika majanga na kuendeleza biashara ili kuona kwamba ipo sawa na uendeshaji wake wa shughuli wa sasa na mbinu za kibiashara.

(5) Mipango iliyotajwa chini ya kanuni ndogo ya (4) itajaribiwa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa mmiliki wa leseni atakuwa na uwezo wa kutekeleza mipango hiyo katika kipindi cha mitikisiko mikali ya biashara.

*GN NO. 478P (Tangazo Linaendelea)*

Kituo cha usimamizi

**12**.-(1) Mmiliki wa leseni atatakiwa kuanzisha na kutunza kituo cha usimamizi chenye makazi ndani ya Tanzania Bara.

(2) Kituo cha usimamizi kinachotajwa chini ya kanuni hii itakuwa na angalau mkurugenzi mmoja na mfanyakazi maalum mmoja, au kama itakavyoamuliwa na Bodi.

Utambulisho wa mchezaji

**13**.-(1) Mchezaji anayedhamiria kushiriki katika mchezo ya kubahatisha, atathibitisha utambulisho wake kwa kuwasilisha moja ya nyaraka zifuatazo kwa mmiliki wa leseni:

(a) hati ya kusafiria;
(b) kitambulisho cha taifa; au
(c) kitambulisho kingine chochote au nyaraka ambayo itaidhinishwa na Bodi.

(2) Mmiliki wa leseni hatakubali dau lolote kutoka kwa mchezaji hadi hapo utambulisho wa mchezaji utakapohakikishwa kwa mujibu wa mifumo ya udhibiti iliyoidhinishwa.

Usajili wa mchezaji

**14**.-(1) Mchezaji atajisajili kwa mmiliki wa leseni kwa kujaza na kuwasilisha fomu ya usajili ambayo itajumuisha:

(a) jina kamili;
(b) jinsi;
(c) nakala ya kitambulisho au namba ya utambulisho au namba ya hati ya kusafiria au uthibitisho mwingine wowote wa utambulisho kama ambavyo Bodi itaidhinisha;
(d) anwani ya makazi na posta;
(e) anwani ya barua pepe;
(f) nambari ya simu;
(g) umri; na
(h) akaunti ya mchezaji iliyochaguliwa.

(2) Mmiliki wa leseni atampatia mchezaji-

*GN NO. 478P (Tangazo Linaendelea)*

(a) vigezo na masharti ya usajili;
(b) kanuni za mchezo kwa michezo iliyoruhusiwa inayotolewa na mmiliki wa leseni;
(c) gharama yoyote inayohusiana na ushiriki katika mchezo; na
(d) tamko la wazi kuhusu wachezaji chini ya umri, kucheza kistaarabu na ujumbe kwamba mchezaji anaweza kuweka mipaka kama ilivyoainishwa katika Sehemu ya Kumi na maelekezo mengine yoyote kama Bodi itakavyoelekeza.

Kukataa kusajili

**15**. Mmiliki wa leseni anaweza kukataa kumsajili mtu kama mchezaji katika mchezo ulioruhusiwa kwa jina lisilofaa, lisilokuwa na maadili au linalovunja sheria.

Akaunti ya kushiriki

**16**.-(1) Mchezaji hatashiriki katika shughuli yoyote ya mchezo wa kubahatisha mtandaoni isipokuwa ameteua akaunti ya benki au taasisi ya kifedha au mwendeshaji wa mtandao wa simu aliyeruhusiwa kwa ajili ya kuwezesha miamala ya kifedha.

(2) Akaunti iliyotajwa chini ya kanuni ndogo ya (1) itateuliwa wakati wa usajili wa mchezaji.

(3) Mmiliki wa leseni hatakubali dau kutoka kwa mchezaji katika mchezo ulioidhinishwa isipokuwa kama akaunti ya mchezaji imefunguliwa kwa jina la mchezaji na kuna fedha za kutosha katika akaunti ya kuweza kulipia kiasi cha dau.

(4) Mchezaji anaruhusiwa kuwa na akaunti moja tu ya mchezaji na mmiliki wa leseni.

(5) Mmiliki wa leseni anaweza kukubali malipo kutoka kwa mchezaji kupitia-

(a) kadi ya malipo;
(b) kadi ya kutolea au akaunti za thamani zilizohifadhiwa;

(c) hamisho la kielektroniki;
(d) hamisho kwa njia ya waya;
(e) hundi;
(f) vocha ya kuongeza fedha;
(g) hamisho kwa njia ya simu; na
(h) njia nyingine yoyote iliyoidhinishwa na Bodi.

Mmiliki wa leseni kutumia akaunti ya mchezaji

**17**. Mmiliki wa leseni anaweza kuifikia akaunti ya mchezaji kwa-
(a) kutoa kiasi cha fedha katika akaunti ya mchezaji kulipia dau;
(b) kuweka kiasi cha fedha alichoshinda mchezaji katika akaunti ya mchezaji;
(c) kuweka bonasi fedha katika akaunti ya mchezaji;
(d) kuhamisha fedha kwenda katika akaunti iliyoteuliwa;
(e) kufunga akaunti ya mchezaji, endapo imebaki bila kutumika kwa kipindi cha zaidi ya siku mia na themanini;
(f) kutekeleza marekebisho yaliyoidhinishwa na uongozi; na
(g) kufanya muamala kama itakavyoelekezwa na Bodi.

Udhibiti wa akaunti ya mchezaji

**18**.-(1) Mmiliki wa leseni ataanzisha mfumo sahihi wa taratibu za udhibiti wa ndani zilizoidhinishwa na Bodi ili kuhakikisha kwamba miamala yote ya akaunti ipo chini ya udhibiti mkali wa usalama na inatunzwa katika kitabu cha kumbukumbu ya ukaguzi wa mfumo.

(2) Pale ambapo mmiliki wa leseni amefunga akaunti ya mchezaji iliyorejelewa chini ya kanuni ya 17(e), atarejesha bakaa yoyote ya fedha zilizosalia kwenye akaunti iliyochaguliwa na mchezaji ndani ya siku tano za kazi.

Michezo iliyokatizwa au kutokufanyika

**19**.-(1) Pale ambapo ushiriki wa mchezaji katika shughuli ya mchezo wa kubahatisha umekatizwa kutokana na tatizo la kimfumo, mmiliki wa leseni anapaswa kujaribu kutatua tatizo kwa kuhakikisha kuwa mfumo unatoa utaratibu kwa mchezaji-

(a) kurejea tena kushiriki katika shughuli ya michezo katika hali ile ile kama ilivyokuwa kabla ya kutokea kwa tatizo wakati mfumo wa michezo ya kubahatisha utakaporejeshwa;

(b) kumaliza mchezo wa kubahatisha ambao haujamalizika; au

(c) kusitisha ushiriki katika mchezo husika.

(2) Pale ambapo ushiriki katika shughuli ya michezo ya kubahatisha hauwezi kuendelea ndani ya muda mahsusi ulioainishwa katika vigezo na masharti, ushiriki katika shughuli ya michezo ya kubahatisha utasitishwa.

(3) Pale ambapo mmiliki wa leseni ameshindwa kutatua tatizo chini ya kanuni ndogo ya (1), atapaswa-

(a) kuitaarifu Bodi juu ya tukio hilo na Bodi inaweza kuchunguza;

(b) kusitisha kufanya shughuli ya michezo ya kubahatisha inayoelekea kuathiriwa na hitilafu au dosari kama hiyo.

(4) Baada ya kuchunguza tukio lililorejelewa chini ya kanuni ndogo ya (3)(a), Bodi inaweza kumuelekeza mmiliki wa leseni-

(a) kurejesha kiasi kilichowekwa kama dau na mchezaji; na

(b) ikiwa mchezaji amepata alama wakati shughuli ya mchezo ilipokatizwa, amlipe mchezaji thamani ya fedha ya alama hizo; au

(c) kuchukua hatua zozote ambazo Bodi inaona inafaa.

## SEHEMU YA TANO
## TUZO

Tuzo ya fedha na isiyo ya fedha

**20**.-(1) Pale ambapo mchezaji atashinda tuzo ya fedha, mmiliki wa leseni ataweka kiasi cha tuzo ya fedha kwenye akaunti ya mchezaji.

(2) Pale ambapo mchezaji ameshinda tuzo isiyo ya fedha, mmiliki wa leseni atapaswa-

(a) kuikabidhi tuzo hiyo yeye binafsi au kwa barua iliyothibitishwa kwa anwani iliyotolewa na mchezaji; au

(b) kumpa mchezaji notisi ya maandishi ya anwani ambayo tuzo inaweza kupokelewa.

Tuzo isiyo ya fedha ambayo haijadaiwa

**21**.-(1) Iwapo tuzo isiyo ya fedha haitachukuliwa ndani ya siku tisini baada ya kutolewa kwa taarifa ya mahali inapopaswa kuchukuliwa, mmiliki wa leseni ataitaarifu Bodi kuhusu tuzo yoyote ambayo haijadaiwa.

(2) Baada ya kupokea taarifa chini ya kanuni ndogo ya (1), Bodi itatoa maelekezo kwa mmiliki wa leseni kutoa tuzo ambayo haijadaiwa kwa mnada wa hadhara, zabuni au kama Bodi itakavyoamua.

(3) Kwa kuzingatia usimamizi wa Bodi, mmiliki wa leseni ataondoa gharama za uondoshaji kutoka katika mapato ya mauzo na kulipa kiasi kitakachobaki katika akaunti ya mchezaji.

(4) Pale ambapo hakuna akaunti ya mchezaji, mmiliki wa leseni ataweka salio katika akaunti ya mchezaji iliyoteuliwa awali.

(5) Pale ambapo mmiliki wa leseni hafahamu mahali mchezaji alipo, mmiliki wa leseni atalipa salio katika akaunti iliyoanzishwa na kutunzwa na Bodi.

Madai ya tuzo ambayo haijalipwa

**22**. Pale ambapo dai la tuzo limetolewa kwa mmiliki wa leseni ndani ya siku tisini baada ya kumalizika kwa shughuli ya michezo ya kubahatisha,

*GN NO. 478P (Tangazo Linaendelea)*

mmiliki wa leseni atatatua dai hilo.

Kutaifishwa kwa tuzo ambazo hazijachukuliwa

**23**. Pale ambapo tuzo haijachukuliwa ndani ya miaka mitatu baada ya kumalizika kwa shughuli ya mchezo wa kubahatisha, stahili hiyo itakatishwa na tuzo kutaifishwa na Bodi.

Kuzuia tuzo

**24**.-(1) Mmiliki wa leseni anaweza kuzuia tuzo katika mchezo endapo ana sababu ya kuamini kwamba:

(a) ushindi uliathiriwa na mwenendo usio halali au usio wa kawaida; au

(b) mchezaji, kwa kitendo cha kukosa uaminifu au kinyume cha sheria kinachoathiri mwenendo au uchezaji wa mchezo, amepata faida kwa ajili yake au mtu mwingine.

(2) Mmiliki wa leseni ambaye amezuia tuzo iliyorejelewa chini ya kanuni ndogo ya (1) atalazimika-

(a) kuitaarifu Bodi kuhusu mazingira ya tukio; au

(b) kusitisha kufanya shughuli za michezo ya kubahatisha ikiwa tukio lililojitokeza chini ya kanuni ndogo ya (1) lina uwezekano wa kujirudia.

(3) Bodi inaweza kupeleleza suala husika na kuelekeza mmiliki wa leseni-

(a) kulipa tuzo;

(b) kurejesha dau lililolipwa;

(c) kubaki na tuzo na kuomba mwongozo wa Bodi; au

(d) kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mchezaji.

Tuzo kuwekwa wazi

**25**. Mmiliki wa leseni ataweka wazi tuzo katika kila mchezo unaotolewa kwa ajili ya kucheza.

## SEHEMU YA SITA
## MIFUMO YA UDHIBITI

Uanzishaji wa mifumo ya udhibiti

**26.**-(1) Mmiliki wa leseni ataanzisha na kudumisha mifumo ya udhibiti kwa madhumuni ya udhibiti wenye ufanisi wa uendeshaji wake.

(2) Mifumo ya udhibiti inayopendekezwa itajumuisha-

(a) mianzi laini ya kompyuta;
(b) taratibu zinazopaswa kufuatwa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za michezo ya kubahatisha;
(c) vigezo na masharti ya mchezo;
(d) taratibu na viwango vya matengenezo, usalama, uhifadhi na usafirishaji wa vifaa vya michezo ya kubahatisha;
(e) taratibu za-
   (i) kurekodi miamala ya michezo ya kubahatisha na malipo ya tuzo;
   (ii) matumizi na matengenezo ya miundombinu ya usalama;
   (iii) kuteua na kufanya ukaguzi wa usalama wa mifumo;
   (iv) utaratibu mwingine wowote ambao Bodi inaweza kuhitaji;
(f) viwango vya kiufundi ambavyo vitajumuisha yafuatayo:
   (i) uzalishaji wa namba bila mpangilio;
   (ii) mfumo wa utoaji taarifa;
   (iii) miundombinu ya mtandao na mifumo ya kompyuta;
   (iv) maombi ya dau;
   (v) uadilifu wa mfumo; na
   (vi) mahitaji mengine yoyote.

Viwango, vipimo na miongozo

**27.**-(1) Bodi itaweka viwango vya kiufundi,

vipimo na miongozo kuhusiana na vifaa na mifumo ya michezo ya kubahatisha.

(2) Vifaa na mifumo ya michezo ya kubahatisha inayotumika katika shughuli ya michezo ya kubahatisha itakuwa sehemu ya mifumo ya udhibiti.

Uidhinishaji wa mifumo ya udhibiti

**28**.-(1) Mmiliki wa leseni atawasilisha maombi kwa Bodi kwa ajili ya kuidhinisha mifumo ya udhibiti siku thelathini kabla ya kuanza kwa shughuli za michezo ya kubahatisha.

(2) Kila mchezo ulioruhusiwa utatumia mifumo ya udhibiti iliyoidhinishwa.

(3) Mmiliki wa leseni atapaswa kuleta maombi ya mabadiliko katika mfumo wa udhibiti kwa ajili ya kuidhinishwa na Bodi.

(4) Mfumo wa udhibiti unaorejewa chini ya kanuni ndogo ya (3) utakuwa na maelezo ya mabadiliko yanayopendekezwa.

Kushindwa kuripoti mabadiliko

**29**. Kwa kuzingatia kanuni ya 26 na pale ambapo kuna kushindwa kuripoti mabadiliko, Bodi inaweza-

(a) kutoa agizo la kurekebisha;

(b) kutoza faini ya shilingi laki tano kwa mmiliki wa leseni kwa kila siku ya kutoripoti mabadiliko; au

(c) kusimamisha au kufuta leseni.

Uamuzi

**30**.-(1) Bodi itashughulikia maombi ya uidhinishaji wa mifumo ya udhibiti na kutoa uamuzi ndani ya siku thelathini baada ya kupokea maombi.

(2) Wakati wa kufanya maamuzi chini ya kanuni ndogo ya (1) Bodi inaweza-

(a) kuidhinisha mfumo wa udhibiti uliopendekezwa au mabadiliko yanayopendekezwa katika mfumo wa udhibiti ulioidhinishwa;

(b) kukataa kuidhinisha mfumo wa udhibiti uliopendekezwa au mabadiliko yanayopendekezwa ya mfumo wa udhibiti ulioidhinishwa; au

(c) kuhitaji maboresho katika mfumo wa udhibiti.

(3) Bodi itamjulisha mmiliki wa leseni kwa maandishi juu ya uamuzi uliofanyika na endapo Bodi imekataa kuidhinisha au kuhitaji maboresho katika mifumo ya udhibiti itaeleza sababu zake.

Maelekezo ya kubadili mfumo wa udhibiti

**31**.-(1) Bodi inaweza kumuelekeza mmiliki wa leseni kubadili mfumo wa udhibiti ulioidhinishwa katika namna ambayo itaelekezwa na Bodi.

(2) Pale ambapo mmiliki wa leseni atashindwa au kukataa kutekeleza maelekezo ya Bodi kama yalivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), idhini ya mfumo wa udhibiti itasitishwa kwa muda au kufutwa.

Viwango vya usanifu, matumizi na utunzaji wa tovuti

**32**.-(1) Ukurasa wa mwanzo wa tovuti au njia nyingine yoyote inayohusiana na hiyo ambayo mchezo utapatikana unapaswa kuwa na taarifa zifuatazo:

(a) jina na anwani iliyosajiliwa ya mmiliki wa leseni;

(b) namba ya leseni na tarehe ya kutolewa kwa leseni;

(c) maelezo kwamba shughuli ya mmiliki wa leseni inadhibitiwa na Bodi;

(d) ufikiaji wa moja kwa moja wa tovuti;

(e) viungo ndani ya tovuti vinavyompeleka mchezaji katika michezo na dau linalotolewa;

(f) viungo katika tovuti vinavyompeleka mchezaji katika taratibu zilizoainishwa na mmiliki wa leseni kwa ajili ya usajili wa mchezaji na udhibiti wa akaunti ya mchezaji;

(g) tamko la kucheza kistaarabu;

(h) dawati la msaada au namba ya bure ya msaada; na

(i) taarifa nyingine yoyote kama Bodi itakavyohitaji.

(2) Mmiliki wa leseni ataonesha katika skrini, kwa muda wote wa mchezo, kaunta ambayo inasasisha automatiki na kuonesha bakaa katika akaunti ya mchezaji.

(3) Mmiliki wa leseni hatakiwi kutoa michezo iliyojaa skrini nzima, isipokuwa kama muda halisi wa mchezo unaoneshwa katika skrini kwa wakati wote na mchezaji anapewa nafasi ya kutoka katika mchezo.

(4) Kwa madhumuni ya kanuni hii, "kaunta" maana yake ni dirisha la mtandaoni katika tovuti au njia nyingine yoyote inayohusiana na hiyo inayoonesha bakaa katika akaunti ya mchezaji.

Viwango vya ulinzi, ufikiaji na utunzaji

**33**.-(1) Mmiliki wa leseni anapaswa kuainisha katika tovuti au njia nyingine inayofanana nayo, michezo ambayo-

(a) imejaribiwa na maabara ya michezo ya kubahatisha iliyotambuliwa;

(b) ni salama na ya kuaminika;

(c) kiwango cha kurudi kwa mchezaji kiwe kimeidhinishwa awali na kukaguliwa; na

(d) imetimiza matakwa mengine kama ambavyo itaamuliwa na Bodi.

(2) Michezo inayorejewa katika kanuni ndogo ya (1), inapaswa kwanza kuidhinishwa na Bodi.

(3) Mmiliki wa leseni anapaswa kuweka skana za virusi na programu nyingine za utambuzi kwenye mifumo ya taarifa.

(4) Programu zinazorejewa katika kanuni ndogo ya (3) zinapaswa kuhuishwa mara kwa mara.

(5) Mmiliki wa leseni ataweka hatua za udhibiti wa mabadiliko katika vifaa na mifumo ya uchakataji wa taarifa ili kupunguza hatari ya usalama au kushindwa

kwa mfumo.

(6) Mmiliki wa leseni atahakikisha kuwa maelezo ya mchezaji yanalindwa dhidi ya matumizi yasiyoruhusiwa.

(7) Mmiliki wa leseni ataweka programu ya ulinzi wa kompyuta na kuhakikisha kuwa una sifa zifuatazo:

(a) masuala yanayohusiana na programu ya ulinzi wa kompyuta yanabaki kwenye mfumo huo;

(b) idadi ndogo ya akaunti zibaki kwenye programu ya ulinzi wa kompyuta;

(c) mifuko yote ya data iliyoelekezwa kwenye programu ya ulinzi wa kompyuta itakataliwa ikiwa utafika kwenye violesura vya mitandao ambayo iko nje ya wastani.

(8) Mmiliki wa leseni atahakikisha programu ya ulinzi inaweza-

(a) kusanifiwa katika namna ambayo viunganishi vyote kwenda na kutoka katika mtandao wa ndani inapitia katika programu ya ulinzi;

(b) kukataa viunganishi vyote isipokuwa vile ambavyo imeidhinishwa maalum na mamlaka husika;

(c) kuwa na uthibitishaji imara wa mtumiaji; na

(d) kuwa na maelezo ya kina katika ngazi ya maombi ikijumuisha michezo iliyofaulu kuwa ya haki na isiyo na mpangilio maalum.

(9) Mfumo wa taarifa utatumia mbinu za historia ya nywila ili kudumisha historia ya nywila za watumiaji, ambayo itakuwa na nywila tatu za mwisho za watumiaji zilizohifadhiwa katika fomu iliyosimbwa.

(10) Nywila ya taarifa katika mfumo itabadilishwa kila baada ya siku tisini.

(11) Mfumo wa taarifa unapaswa-

(a) kutoa namna kwa watumiaji kubadili nywila

zao;

(b) kuzuia mwangwi wa nywila inapoingizwa; na

(c) kupunguza idadi ya majaribio ya kuingia yaliyofeli hadi matatu na kiwango ambacho majaribio ya kuingia yanaweza kufanywa hadi dakika kumi.

(12) Bodi itakuwa na mamlaka ya kutoa miongozo ya viwango vinavyohusiana na Sehemu hii.

## SEHEMU YA SABA
## UDHIBITI WA NDANI

Uanzishaji wa utaratibu wa udhibiti wa ndani

**34**.-(1) Mmiliki wa leseni ataanzisha na kutunza mfumo wa utaratibu wa udhibiti wa ndani.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mfumo wa utaratibu wa udhibiti wa ndani utajumuisha utawala na taratibu za kihasibu kwa ajili ya udhibiti wenye ufanisi wa masuala ya ndani ya mmiliki wa leseni.

(3) Mfumo wa utaratibu wa udhibiti wa ndani utahakikisha kwamba-

(a) mali za mmiliki wa leseni zinalindwa;

(b) udhibiti wa fedha upo;

(c) taarifa za fedha ni sahihi na uhakika;

(d) miamala iliyofanywa ni kwa mujibu wa kibali na idhini ya uongozi;

(e) miamala inarekodiwa kwa uangalifu ili kuhakikisha tathmini sahihi ya mapato, ada na ushuru wa michezo ya kubahatisha;

(f) kazi, wajibu na majukumu yametengwa na kutekelezwa ipasavyo.

Uidhinishaji wa utaratibu wa udhibiti wa ndani

**35**.-(1) Mmiliki wa leseni atapaswa, kabla ya kuanza kwa utekelezaji, kuwasilisha maombi kwa Bodi kwa ajili ya kuidhinisha mfumo wa udhibiti wa ndani.

(2) Mfumo wa udhibiti wa ndani unaopendekezwa utajumuisha:

*GN NO. 478P (Tangazo Linaendelea)*

(a) chati ya shirika;
(b) maelezo ya majukumu na wajibu wa kila nafasi iliyooneshwa kwenye chati ya shirika;
(c) mifumo na taratibu za uhasibu na chati ya hesabu;
(d) mifumo na taratibu za utawala;
(e) mianzi laini ya kompyuta;
(f) taratibu za jumla zinazopaswa kufuatwa katika uendeshaji wa michezo;
(g) taratibu na viwango vya matengenezo, usalama, uhifadhi na usafirishaji wa vifaa vya michezo ya kubahatisha; na
(h) taratibu za-
   (i) kunakili miamala ya michezo na malipo ya wachezaji walioshinda;
   (ii) matumizi na matunzo ya miundombinu ya ulinzi;
   (iii) kuzuia wachezaji walio chini ya umri kushiriki katika michezo ya kubahatisha;
   (iv) kubaini na kuzuia utakasishaji fedha haramu; na
   (v) taarifa nyingine kama ambavyo Bodi itahitaji.

(3) Bodi itapaswa, ndani ya muda unaofaa, kushughulikia maombi yaliyowasilishwa katika kanuni hii na kutoa uamuzi kwa-
(a) kuidhinisha mfumo wa utaratibu wa udhibiti wa ndani unaopendekezwa;
(b) kukataa mfumo wa utaratibu wa udhibiti wa ndani unaopendekezwa; au
(c) kuomba taarifa za ziada.

(4) Katika kuzingatia maombi, Bodi inaweza kuwasilisha mfumo wa utaratibu wa udhibiti wa ndani unaopendekezwa kwa ajili ya majaribio kwa wakala aliyeidhinishwa.

(5) Endapo maombi ya idhini ya mfumo wa

utaratibu wa udhibiti wa ndani yamekataliwa, Bodi itamtaarifu mmiliki wa leseni kwa maandishi na kutoa sababu za uamuzi wake wa kukataa maombi hayo.

(6) Pale ambapo Bodi inaamini kwamba maombi yanaweza kurekebishwa kuweza kupelekea kutolewa kwa idhini, itaelezea namna ambavyo maombi yanapaswa kurekebishwa na kuwasilishwa tena.

Urekebishaji wa utaratibu wa udhibiti wa ndani ulioidhinishwa

**36**. Mmiliki wa leseni atapaswa kuwasilisha kwa Bodi maombi ya kufanya marekebisho ya mfumo wa taratibu za udhibiti wa ndani kwa maandishi ambapo Bodi itashughulikia maombi hayo na kutoa uamuzi kwa mujibu wa kanuni ya 35(3).

## SEHEMU YA NANE
## UTOAJI TAARIFA KWA MIAMALA SHUKU

Kanuni na taratibu za miamala shuku

**37**.-(1) Mmiliki wa leseni anapaswa kuandaa kanuni na taratibu zitakazoidhinishwa na Bodi ili kumuwezesha kutambua na kudhibiti miamala shuku inayohusiana na uwekaji na utoaji wa fedha kutoka katika akaunti ya mchezaji.

(2) Kanuni na taratibu zinazorejewa katika kanuni ndogo ya (1) zitajumuisha-

(a) masharti kwa mmiliki wa leseni kujua wachezaji wake;

(b) itifaki za mwenye leseni kutambua, kushughulikia na kuzuia miamala shuku; na

(c) mfumo wa kufuatilia na kuripoti miamala shuku kwa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu kuhusu akaunti za wachezaji na kuiarifu Bodi.

(3) Mfumo wa udhibiti unaorejewa katika kanuni ndogo ya (2)(c) inapaswa kuweza kutambua-

(a) shughuli zinazoweza kuhusiana na utakasishaji fedha haramu kwa kuchanganua miamala na wasifu wa watumiaji kwa wakati

halisi na kuwahusisha wale walio na wasifu wa viashiria hatarishi;

(b) mifumo isiyo ya kawaida ya kubeti inayohusishwa na utakasishaji fedha haramu; na

(c) majaribio ya kukwepa ukomo wa dau lililowekwa.

(4) Mmiliki wa leseni atateua mtu ambaye atawajibika kuripoti miamala shuku.

Wajibu wa kuripoti miamala shuku

Sura ya 423

**38**. Pale ambapo mmiliki wa leseni anapotambua au kushuku uwepo wa miamala shuku ambayo inahusisha utakasishaji fedha haramu au makosa yanayohusiana, anapaswa kuripoti tukio hilo kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti Utakasishaji wa Fedha Haramu.

## SEHEMU YA TISA
## ULINZI WA MCHEZAJI

Ulinzi kwa watoto

**39**.-(1) Mmiliki wa leseni atawajibika kama sehemu ya mifumo yake ya udhibiti kuweka mifumo madhubuti ya kuhakikisha wachezaji walio chini ya umri wa miaka kumi na nane hawashiriki katika shughuli ya michezo ya kubahatisha.

(2) Kwa madhumuni ya masharti ya kanuni hii, Bodi inaweza kuelekeza mmiliki wa leseni kurekebisha mifumo yake au kuweka mifumo mipya pale ambapo haijaridhika na mifumo iliyopo.

Urudishaji wa fedha

**40**.-(1) Mmiliki wa leseni anapaswa kuhakikisha anazuia ushiriki au madai ya tuzo kwa watu walio chini ya umri wa miaka kumi na nane.

(2) Mmiliki wa leseni atatuma kwa Bodi kila robo mwaka asilimia ishirini na tano ya jumla ya thamani ya tuzo ambazo hazijadaiwa kuwa sehemu ya fedha ya Bodi.

*GN NO. 478P (Tangazo Linaendelea)*

(3) Mmiliki wa leseni atabaki na asilimia sabini na tano ya jumla ya thamani ya tuzo ambazo hazijadaiwa ambazo zitapaswa kutumiwa na mmiliki wa leseni kama sehemu ya fedha za kushindaniwa katika jakipoti ya ahadi.

Usajili

**41**.-(1) Mmiliki wa leseni atasajili mtu kama mchezaji baada ya kupokea ombi la usajili.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mmiliki wa leseni atakataa ombi la usajili ambalo taarifa zake hazijakamilika.

Vigezo na masharti

**42**. Mmiliki wa leseni atahakikisha vigezo na masharti ya kila mchezo yanakuwa wazi na mafupi yenye kueleweka.

Ukiukwaji wa kanuni

**43**.-(1) Michezo yote na matukio ya kubeti yatafuata seti za kanuni za kawaida na hayatakiuka kanuni hizo.

(2) Mabadiliko ya kanuni zozote zinazorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1), yatajumuisha mchezo tofauti au tukio la kubeti, endapo tofauti za idadi ya juu zaidi ya madau kwa kila mchezo zinaruhusiwa.

Utenganishaji wa akaunti

**44**. Mmiliki wa leseni atahakikisha kwamba madeni yake na bakaa ya akaunti ya mchezaji vinatenganishwa wakati wote.

Marekebisho ya akaunti ya mchezaji

**45**. Pale ambapo kuna marekebisho yoyote yaliyofanywa katika akaunti ya mchezaji, marekebisho hayo yatakaguliwa na kuidhinishwa na msimamizi aliyeidhinishwa.

Utoaji wa mikopo

**46**. Mmiliki wa leseni hatatoa mkopo kwa mchezaji au akaunti ya mchezaji au kuwa wakala kwa mtoa mikopo ili kuwezesha utoaji wa mkopo kwa mchezaji au akaunti ya mchezaji, isipokuwa kama

imeidhinishwa na Bodi.

## SEHEMU YA KUMI
## WAJIBU WA KUCHEZA KISTAARABU

Notisi ya onyo

**47**.-(1) Mmiliki wa leseni anapaswa kuonyesha kiunganishi katika tovuti chenye notisi ya onyo-

(a) juu ya uwezekano wa uraibu; na

(b) kwa madhara kama hayatadhibitiwa na kuwekwa kwa kiasi.

(2) Mmiliki wa leseni atahakikisha kuwepo kwa wafanyakazi wa kutosha ambao wamefunzwa ipasavyo kufuatilia na kutoa ushauri kuhusu matatizo yatokanayo na michezo ya kubahatisha.

(3) Ukurasa wa mbele wa tovuti ya mmiliki wa leseni au njia nyingine yoyote inayohusiana, itaonesha kwa uwazi kiungo kitakachompeleka mchezaji katika sera ya wajibu wa kucheza kistaarabu michezo ya kubahatisha na notisi inayomwelekeza mchezaji kwa mtaalamu.

(4) Sera ya wajibu wa kucheza kistaarabu michezo ya kubahatisha itajumuisha yafuatayo:

(a) taarifa kuhusu matatizo yatokanayo na michezo ya kubahatisha na kiungo cha kupata taarifa hiyo;

(b) taarifa za kituo cha huduma kwa wateja na timu ya ndani ya usaidizi inayomshughulikia mchezaji mwenye tatizo litokanalo na michezo ya kubahatisha;

(c) orodha ya hatua za ulinzi wa mchezaji ambazo zinapatikana kwenye tovuti na ufikiaji wa hatua hizi;

(d) kiungo kinachompeleka mchezaji katika mchakato rahisi wa kujitathmini ili kubaini uwezekano wa viashiria hatarishi; na

(e) taarifa na viungo vinavyompeleka mchezaji katika tovuti ya Bodi.

(5) Ukurasa wa mbele wa tovuti ya mmiliki wa leseni au njia nyingine zinazohusiana zinapaswa:

(a) kuonyesha wazi notisi inayosema kwamba hakuna mchezaji aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane anayeruhusiwa kushiriki katika shughuli za michezo ya kubahatisha;

(b) kutoa kiungo cha programu ya kuchuja ambayo inazuia watoto kufikia shughuli za michezo ya kubahatisha.

(6) Ukurasa wa michezo isiyolipishwa ya mmiliki wa leseni utatoa kizuizi sawa cha umri, wajibu wa kucheza kistaarabu michezo ya kubahatisha, maelezo ya ulinzi wa mchezaji na viungo kwenye mchezo halisi wa pesa.

Kujiondoa

**48**.-(1) Mfumo wa udhibiti wa mmiliki wa leseni utapaswa, kwa maombi ya mchezaji, kumwondoa mchezaji asishiriki katika shughuli ya mchezo wa kubahatisha.

(2) Mmiliki wa leseni atarekodi kwa usahihi na kuhifadhi sababu za ombi la mchezaji kujiondoa.

(3) Mchezaji hatarejeshwa kwa muda wa miezi sita kuanzia tarehe ya kujiondoa isipokuwa imeidhinishwa na Bodi.

Taarifa za mchezaji kuondolewa

**49**.-(1) Mmiliki wa leseni ataonyesha kwa uwazi kwenye tovuti au njia nyingine yoyote inayohusiana, sehemu ambayo mchezo hupatikana, viungo au ufikiaji wa taarifa na fomu zitakazotumiwa na mtu ambaye anataka kujiandikisha kama mtu aliyeondolewa chini ya kanuni ya 48.

(2) Kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), ukurasa wa mbele wa tovuti ya mmiliki wa leseni utaonyesha wazi kiungo kitakachompeleka mchezaji katika sera ya wachezaji kujiondoa.

(3) Mmiliki wa leseni hatatuma matangazo ya michezo ya kubahatisha kwa mchezaji ambaye

ameondolewa kwenye shughuli ya michezo ya kubahatisha katika kipindi cha kuondolewa.

Ukomo wa kubeti au dau

**50**.-(1) Mmiliki wa leseni ataruhusu mchezaji kuweka kikomo cha kiasi ambacho mchezaji anaweza kuweka katika akaunti yake au dau.

(2) Mchezaji ambaye ameweka kikomo kinachorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1), anaweza kurekebisha au kubatilisha kikomo baada ya kuidhinishwa na mmiliki wa leseni.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (2), marekebisho au kubatilisha kikomo hakutatekelezwa isipokuwa hadi siku saba za kalenda zimepita.

(4) Mmiliki wa leseni hatakubali dau kutoka kwa mtu au mchezaji ambaye amerekebisha au kubatilisha kikomo cha kiasi ambacho mchezaji anaweza kuweka katika akaunti ya mchezaji au kuweka dau isipokuwa hadi siku saba za kalenda zimepita.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## KUMBUKUMBU ZA HESABU NA RITANI

Kumbukumbu za hesabu

**51**.-(1) Kila mmiliki wa leseni atatunza kumbukumbu sahihi, kamili zinazosomeka na za kudumu za miamala yote inayohusu shughuli zote za michezo ya kubahatisha kwa namna ambayo Bodi itaidhinisha.

(2) Kila mmiliki wa leseni ya kasino, mashine za sloti, bingo, msambazaji, mwendeshaji wa bahati nasibu ya taifa na bahati nasibu nyinginezo ataweka kumbukumbu za jumla za uhasibu katika mfumo wa uhasibu wa kuingiza mara mbili akitunza kumbukumbu za kina zinazosaidia taarifa ndogondogo ikijumuisha kumbukumbu zinazohitajika ama kwa viwango vya chini vya mfumo wa udhibiti wa ndani au mfumo wa udhibiti wa ndani wa mmiliki wa leseni.

(3) Endapo mmiliki wa leseni atashindwa

kutunza kumbukumbu za kukokotoa mapato ya jumla ya michezo ya kubahatisha au ada au tozo zozote zinazotumika, Bodi inaweza kukokotoa na kuamua kiasi cha tozo kwa kuzingatia ukaguzi uliofanywa au taarifa zozote zinazomilikiwa na Bodi au juu ya uchambuzi wa takwimu.

Taarifa za fedha zilizokaguliwa

**52.-**(1) Kila mmiliki wa leseni atapaswa, kwa ajili ya kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (3), baada ya kila mwaka wa fedha kuisha, kuandaa taarifa za kifedha za mwaka kwa mujibu wa viwango vya uhasibu wa fedha Tanzania.

(2) Kila mmiliki wa leseni atatumia mhasibu na mkaguzi huru aliyesajiliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu ambaye atakagua taarifa za mwaka kwa mujibu wa viwango vya ukaguzi vinavyokubalika kwa ujumla.

(3) Kila mmiliki wa leseni atawasilisha kwa Bodi nakala tatu za taarifa za fedha za mwaka zilizokaguliwa na ripoti yoyote inayotoa taarifa ya matokeo ya ukaguzi ikijumuisha ripoti ya ukaguzi wa menejimenti kabla ya siku mia na themanini baada ya kufungwa kwa mwaka wa fedha wa mmiliki wa leseni.

(4) Bodi inaweza kuhitaji maelezo ya ziada au nyaraka kutoka kwa mmiliki wa leseni au mkaguzi wa miliki wa leseni kuhusu taarifa za fedha au huduma zinazofanywa na mkaguzi.

Taratibu za ukaguzi wa Bodi

**53**.-(1) Bodi itafanya ukaguzi wa mara kwa mara wa utendaji kazi au mapitio ya vitabu na kumbukumbu za wamiliki wa leseni.

(2) Mwishoni mwa kila ukaguzi, kitengo cha ukaguzi cha Bodi kitapitia matokeo ya ukaguzi na mmiliki wa leseni. Mmiliki wa leseni anaweza, ndani ya siku kumi za kupitia, kuwasilisha sababu zilizoandikwa kwa nini matokeo ya ukaguzi yasikubaliwe. Bodi itazingatia uwasilishaji kabla ya

uamuzi wake.

Ritani na uwasilishaji wa ritani ya kila mwezi
TS. Na 385 la 2003

**54.**-(1) Pamoja na kodi inayolipwa chini ya Sheria, kila mmiliki wa leseni atalipa ushuru wa michezo ya kubahatisha iliyoidhinishwa na Bodi katika Jedwali la Kwanza la Kanuni za Michezo ya Kubahatisha.

(2) Ritani na uwasilishaji wa ritani ulioainishwa katika Sheria na Kanuni za Michezo ya Kubahatisha zitawasilishwa kwa Bodi kabla ya tarehe iliyotajwa katika Sheria.

(3) Nakala za fomu za ritani ya kodi itokanayo na michezo ya kubahatisha ya kila mwezi zilizokusanywa na Kamishna zitawasilishwa kwa Bodi ndani ya siku saba baada ya kodi hiyo kulipwa.

Taarifa za fedha za uongo au za kupotosha

**55.** Mmiliki wa leseni ambaye atawasilisha taarifa ya fedha huku akijua kuwa ni ya uongo au ya kupotosha atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## MASHARTI YA JUMLA

Matangazo kwenye shughuli zenye leseni

**56**.-(1) Mtu hatatangaza shughuli za michezo ya kubahatisha isipokuwa kama ameidhinishwa na Bodi.

(2) Mmiliki wa leseni atatayarisha kanuni za utendaji zinazohusu utangazaji na mahusiano ya umma kuhusiana na shughuli ya michezo ya kubahatisha ambayo itawasilishwa kwa Bodi ili kuidhinishwa.

(3) Tangazo lolote la michezo ya kubahatisha linaweza kuchunguzwa na Bodi na endapo Bodi itajiridhisha kuwa tangazo hilo halifai itamtaka mmiliki wa leseni kuliondoa tangazo hilo.

(4) Kwa madhumuni ya Kanuni hizi, matangazo

yasiyofaa yanajumuisha:

(a) matangazo yenye kuvunja sheria;
(b) matangazo yenye kupotosha;
(c) matangazo yasiyo na maadili;
(d) matangazo yasiyojikita katika jambo lililotendeka; na
(e) matangazo ya uongo, yenye kuhadaa.

Kanuni kutangazwa kwa Kiswahili na Kiingereza

**57**. Mmiliki wa leseni ataweka katika tovuti yake au katika njia nyingine yoyote, kanuni zinazohusiana na mchezo wa kubahatisha katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza au lugha nyingine yoyote iliyoidhinishwa na Bodi.

Dhamana ya benki

**58.-**(1) Kila kasino itadumisha katika namna na kiwango kama itakavyoidhinishwa au kuhitajika na Bodi, fedha taslimu au sawa na fedha taslimu katika kiasi kinachojitosheleza kuwalinda wachezaji dhidi ya kushindwa kulipa madeni ya michezo ya kubahatisha anayodaiwa mmiliki wa leseni.

TS. Na. 385 la 2003

